# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA UCHUMI YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA AFISI YA RAIS, KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI

KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

Mheshimiwa Spika,

Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujaalia uzima na Afya njema tukaweza kukutana tena katika Baraza hili tukufu kwa ajili ya kuendelea kuwatumikia wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika,

Nichukue fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia fursa hii adhimu na muhimu ya kuwasilisha maoni ya Kamati ya Uchumi juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika,

Kwa namna ya pekee nachukua fursa hii kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa ujasiri wake wa kutekeleza vyema jukumu zima la uongozi wa nchi yetu sambamba na jitihada anazochukua za kuendeleza Uchumi na Uwekezaji na sekta nyengine hapa nchini. Ni dhahiri kuwa, uimara wa sekta hizo ndio utakaopelekea kupiga hatua ya kimaendeleo na kuimarisha uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika,

Kamati yangu inatoa shukurani za dhati kwa Mheshimiwa Makamo wa kwanza wa Rais kwa kushauriana vyema na Mheshimiwa Rais kwenye masuala mbali mbali ya uendeshaji wa nchi yetu kwa hekima na busara ya hali ya juu.

Aidha, tunamshukuru Makamo wa Pili wa Rais, Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdullah kwa busara zake na ushauri anaompatia Mheshimiwa Rais katika utekelezaji wa mambo mbali mbali kwa ustawi wa nchi hii na wananchi wake.

Mheshimiwa Spika,

Kamati yangu inatoa shukurani kwa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa ushirikiano anaoupatia Kamati katika utekelezaji wa majukumu yake kwa Wizara yake. Kwa kweli, Kamati imeridhishwa na ushiriki wa Mheshimiwa Waziri kwenye shughuli zake zilizopelekea kuwa na uelewa mpana wa mafanikio na changamoto za taasisi zake.

Mheshimiwa Spika,

Kwa heshima na taadhima, na kwa kuthamini michango na ushauri mkubwa katika kutekeleza kazi za Kamati hii, naomba sasa niwatambue kwa kuwataja majina yao Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Uchumi kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Sabiha Filfil Thani - Mwenyekiti
2. Mhe. Dkt. Soud Nahoda - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Rukia Omar Ramadhan - Mjumbe
4. Mhe. Hassan Hamad Omar - Mjumbe
5. Mhe. Panya Ali Abdalla - Mjumbe
6. Mhe. Ameir Abdalla Ameir - Mjumbe

Mheshimiwa Spika,

Katika uchambuzi wa mafungu haya, Kamati yangu ilifanya kazi na makatibu wetu ambao kwa kiasi kikubwa wamekuwa wakitusaidia na kuturahisishia kuyapitia mafungu ya bajeti hiyo ipasavyo, naomba nao niwatambue kwa kuwataja majina yao kama ifuatavyo;

1. Ndugu Nouman Thabit Nouman -Katibu
2. Ndugu Asma Ali Kassim -Katibu.

Mheshimiwa Spika,

Kutokana na muundo wa Wizara hii kuwa na Makatibu Wakuu wawili (anaeshughulikia Uchumi na Uwekezaji) na (anaeshughulikia Kazi na Uwezeshaji), Kamati imeridhishwa na hatua ya Serikali kuipatia Wizara mafungu mawili ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ili kila Katibu Mkuu aweze kusimamia shughuli zake kwa ufanisi. Kwa mnasaba huo, siku ya Jumatano tarehe 20 Aprili, 2022 Kamati yangu ilipata fursa ya kupitia fungu A07 (Kazi na Uwezeshaji) na fungu A08 (Uchumi na Uwekezaji) na kuyakubali makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii pamoja na marekebisho madogo iliyoyapendekeza.

Fungu A07 (Kazi na Uwezeshaji)

PROGRAMU KUU YA USIMAMIZI WA SHERIA ZA KAZI, UKAGUZI

KAZI NA KAZI ZA STAHA KWA WOTE

Mheshimiwa Spika,

Kamati yangu iliarifiwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023, fungu A07 linaloshughulikia Kazi na Uwezeshaji limekadiriwa kutumia jumla ya shilingi za kitanzania bilioni 34,870,120,000 kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake za msingi.

Mheshimiwa Spika,

Kwa ujumla, programu hii inakadiriwa kupatiwa ruzuku ya jumla ya shilingi za Kitanzania bilioni 1,529,000,000 ambayo ni mapungufu makubwa kutoka kwenye ruzuku iliyokadiriwa kwa mwaka 2021/2022 ambayo ni shilingi za Kitanzania bilioni 2,236,900,000. Mapungufu haya yatazorotesha ukusanyaji wa mapato kupitia shughuli za programu hii kutokana na uhaba wa vitendea kazi vitakavyonunuliwa na hivyo kupelekea Serikali kuu nayo kukosa mapato yanayostahiki.

Mheshimiwa Spika,

Kamati yangu ilipata ukakasi juu ya makadirio hafifu ya fedha zitakazokusanywa na Kamisheni ya Kazi kwa mwaka 2022/2023 na kuarifiwa kuwa, kwa mwaka huo wa fedha, shughuli za

ukadiriaji wa mapato zilifanyika kwa mashirikiano ya pamoja baina ya Wizara husika na watendaji wa Wizara inayohusika na Fedha. Suala hilo ni muhimu katika kuweka malengo sahihi kwa Wizara yanayotekelezeka na kuwa na takwimu sahihi kwa matumizi ya Serikali.

Mheshimiwa Spika,

Mfumo unaotumiwa na Wizara kwa hivi sasa ni wa kuchanganya makadirio ya mapato kwa Unguja na Pemba. Hivyo, Kamati yangu inashauri mfumo huo ufanyiwe marekebisho ili kutoa fursa ya kupima kasi ya kiutendaji baina ya pande mbili hizi na kubuni mikakati mipya pale ambapo malengo hayakufikiwa.

Mheshimiwa Spika,

Kupitia programu ndogo ya Maendeleo ya Ushirika (A0712), Kamati inaipongeza Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa kuongeza maradufu makadirio ya mapato kutoka Shilingi za kitanzania milioni 30,000,000 mwaka huu hadi kufikia Shilingi za kitanzania milioni 80,000,000 kwa mwaka 2022/2023. Hatua hii ni muhimu katika kuhakikisha malengo ya Wizara na Taifa kwa jumla yanatimia.

Mheshimiwa Spika,

Programu ndogo ya Usalama na Afya Kazini inakadiriwa kukusanya jumla ya shilingi za kitanzania milioni 450,000,000 kwa mwaka wa fedha 2022/2023, ikiwa ni upungufu mkubwa kutoka kwenye makusanyo ya mwaka uliotangulia. Hali hii imechangiwa na upungufu wa vifaa vya ukaguzi kwa ajili ya kutoa huduma kwa taasisi mbali mbali na upungufu wa wataalamu wa ukaguzi na hivyo kushindwa kufanya shughuli ya ukaguzi kwa ufanisi jambo ambalo linaziweka rehani afya za wananchi wetu ambao wanahudumia sekta mbali mbali za kiuchumi nchini.

Aidha, Kamati inaiomba Serikali kulipa uzito unaostahiki ombi la Wizara la kujengewa jengo la Uchunguzi wa Wafanyakazi ili kufuatilia kwa karibu zaidi afya za watu wetu wanaojishughulisha na harakati tofauti za kiuchumi.

## PROGRAMU KUU YA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

Mheshimiwa Spika,

Programu hii inalenga kuwapatia Wazanzibari shughuli za kiuchumi na kuwawezesha kumudu mahitaji yao ya msingi. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, programu ndogo ya (SA070301) ya Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi haikutengewa fedha

nyingi kwa ajili ya kufanya matumizi. Kamati yangu iliarifiwa kuwa mfuko uko katika hali nzuri ya kifedha kwa sasa ambapo jumla ya Shilingi za Kitanzania bilioni 37,880,000,000 zinatarajiwa kutumika kwa shughuli mbali mbali za mfuko na kusisitiza kwamba fedha hizo zitumike kama zilivyopangiwa.

Mheshimiwa Spika,

Pamoja na lengo zuri la Wizara kupitia program hii, Kamati yangu inasisitiza suala zima la utolewaji wa taaluma ya uendelezaji wa fedha za mikopo kwa wajasiriamali wetu kabla ya kuwapatia mikopo hiyo ili wapate kunufaika nazo na kuzirudisha kwa wakati kwa ajili ya kupatiwa wajasiriamali wengine.

Aidha, ufuatiliaji wa mara kwa mara unahitajika ili kuona kwa namna gani taaluma iliyotolewa kwa wajasiriamali hao inafanyiwa kazi katika kuendeleza shughuli zao.

Vilevile, Kamati inawaomba viongozi wa kisiasa washauriane na Wizara hii kila wanapohitaji kufanya maamuzi yanayuhusu wajasiriamali ili wapatiwe miongozo stahiki kwa maendeleo yao na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika,

Programu kuu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (PA0703)

imeongezeka maradufu kutoka shilingi za Kitanzania Bilioni 7,634,816,000 mwaka uliopita hadi kufikia shilingi za Kitanzania bilioni 29,377,207,000 kwa mwaka 2022/2023. Kamati yangu iliarifiwa kuwa hali hiyo imetokana na mahitaji ya msingi ya uanzishwaji wa Wakala wa Uwezeshaji wananchi kiuchumi ambayo sheria yake imepitishwa hivi karibuni na Baraza hili. Tunaipongeza Serikali kwa kuandaa mazingira mazuri ya uanzishwaji wa wakala huo kwa wakati.

PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA AFISI YA RAIS, KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI

Mheshimiwa Spika,

Kushuka kwa Makadirio ya matumizi ya kifungu (PA0705) program ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji ni jambo lililoitia wasiwasi Kamati yangu ambapo ilihoji juu ya uwezekano wa Wizara kumudu gharama za uendeshaji kwa mwaka huu wa fedha. Jumla ya shilingi za Kitanzania bilioni 5,388,483,000 zinakadiriwa kupungua kutoka kwenye program hii ambayo mwaka 2021/2022 ilikadiriwa kupatiwa shilingi za Kitanzania bilioni 9,352,396,000. Kutokana na hali hiyo, Kamati ya Uchumi inaishauri Serikali Kuipatia Afisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji fedha zaidi kwa ajili ya kutekeleza

majukum yake kwa ufanisi.

Fungu A08 (Uchumi na Uwekezaji)

Mheshimiwa Spika,

Kamati yangu iliarifiwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023, fungu A08 linaloshughulikia Uchumi na Uwekezaji limekadiriwa kutumia jumla ya shilingi za kitanzania bilioni 19,714,840,000 kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake. Tunaipongeza Wizara kwa kutenga fungu hilo ili kuziwezesha shughuli za Uchumi na Uwekezaji kufanyika kwa ufanisi.

PROGRAMU KUU YA KUIMARISHA UWEKEZAJI NA MASHIRIKIANO BAINA YA SEKTA YA UMMA NA SEKTA BINAFSI

Mheshimiwa Spika,

Mashirikiano ya dhati baina ya sekta ya umma na sekta binafsi ndio chachu ya maendeleo endelevu kwa nchi yetu. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Programu ndogo ya mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi inakadiriwa kutumia jumla ya shilingi za kitanzania milioni 478,384,000. Fedha hizo ni chache

kulingana na jukumu linalobebwa na programu hiyo ndogo kwa uchumi wa nchi yetu. Aidha, Kamati yangu ilishangazwa na maelezo ya kwamba suala la kufanya upembuzi yakinifu kwa miradi inayotaka kuwekezwa nchini halikutengewa fedha na badala yake mwekezaji mwenyewe ndiye anaehitajika kufanya upembuzi yakinifu. Kimsingi, shughuli hiyo ni nyeti na tunaishauri Serikali kulitekeleza jukumu hilo kwa uendelezaji bora wa sekta ya Uwekezaji nchini.

Mheshimiwa Spika,
Kamati yangu iliarifiwa kuwa huduma ya Ushajiishaji na Uwekezaji wa ndani na nje imetengewa jumla ya shilingi za kitanzania bilioni 17,886,800,000 kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Tunaipongeza Wizara kwa kuona umuhimu wa kuendeleza mipango yake ya ujenzi wa miundombinu kwenye maeneo Huru ya Uwekezaji ya Micheweni jambo ambalo litawavutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi na kuyafungua maeneo hayo kimaendeleo. Sambamba na hayo, Kamati inashauri suala la uwekaji wa uzio kwenye eneo hilo na maeneo mengine ya Uwekezaji kupewa kipaumbele maalum ili kuyahifadhi zaidi.

PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA AFISI YA

RAIS –KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI

Mheshimiwa Spika,

Kamati yangu iliarifiwa kuwa jumla ya Tafiti tatu (3) za Uchumi na Uwekezaji zinatarajiwa kufanywa na Wizara kwa mwaka 2022/2023 na kugharimu jumla ya shilingi za kitanzania milioni 313,154,000 na kushauri matokeo ya tafiti hizo yafanyiwe kazi kikamilifu kwa mustakbali mwema wa Uwekezaji nchini na kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika,

Kwa vile Kamati yangu ya Uchumi imepitia, imejadili na kuyakubali mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2022/2023, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili watumie fursa hii kuijadili, kutoa mapendekezo yao na hatimae kuiunga mkono na kuipitisha Bajeti hii ili kumruhusu Mheshimiwa Waziri kutekeleza yale waliyojipangia katika mwaka ujao wa Fedha.

Mheshimiwa Spika,

Kwa niaba ya Kamati yangu Naomba pia kukutakieni sikukuu njema ya Eid-el-Fitry Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu pamoja na wananchi wote wa Zanzibar kwa ujumla. Naunga mkono hoja na Naomba kuwasilisha.

Ahsante sana,

……………………………,

Mhe. Sabiha Filfil Thani,

Mwenyekiti,

Kamati ya Uchumi,

Baraza la Wawakilishi,

Zanzibar.